



Uchunguzi Kisemiotiki wa Athari za Kihistoria na Kimazingira kwa Uchumi na Maisha ya Kijamii katika Pwani ya Kenya

Leonard Sanja, Evans Mbuthia*

Idara ya Isimu Na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi, Kenya

IKISIRI

Makala hii inachunguza athari za kimazingira kwa jamii za pwani ya Kenya tangu karne ya 18 walipokuja Waarabu, Waingereza kuanzia 1895 hadi sasa baada ya Kenya kupata uhuru. Ili kukuza mjadala, makala hii ilifafanua ishara na tamathali za lugha zinazohusu mazingira katika semi na ushairi wa Kivumba kwa kutumia nadharia ya semiotiki. Uchunguzi ulijikita katika misimbo ya Barthes (1957) ya kiseme, kiishara na kirejelezi kwa kutumia mbinu ya kimaielezo. Kufafanua tamathali za lugha pamoja na ishara katika matini za kifasihi ni njia bora ya kudhihirisha ujumbe unaowasilishwa kwa msomaji wa kifasihi (Bradford, 1997; Wamitila, 2003; Wales, 2011). Makala hii inajadili kwamba, semi na ushairi kama vipengele vya fasihi simulizi, vinaweza kuwa chombo mbadala cha kuainishia taswira kamili kuhusu athari za muda mrefu za kimazingira kwa jamii za pwani ya Kenya. Makala inahitimisha kwamba, Athari za kimazingira kwa jamii za pwani ya Kenya ni dhahiri na suluhu ya haraka inahitajika. Wengi wanaishi kwa umaskini na kukosa maslahi ya kimsingi kama maji ya kunywa. Kuna uhaba wa chakula na ndoa zimeathirika. Maeneo mengi vilevile yanashuhudia mafuriko ya mara kwa mara na ajira haipatikani.

KUHUSU MAKALA

Maneno Muhimu:

Mazingira,
Uchumi,
Semi,
Ushairi,
Semiotiki.

Historia ya Makala:

Tarehe ya Kutumwa: 10 Mei 2025
Tarehe ya Kurekebisha: 5 Juni 2025
Tarehe ya Kukubalika: 5 Julai 2025
Mtandaoni: 28 Agosti 2025

1. Utangulizi

Fasihi simulizi hutumia lugha ya kitamathali kwa wingi kuliko tanzu nyingine (Leech & Short, 2007). Lugha ya kitamathali huwasilisha maana nasibishi ya ishara ambazo ni za kina. Ushairi na semi huwa na mchango mkubwa katika kuzungumzia masuala mbalimbali yanayoikumba jamii. Fasihi ya lahaja yoyote hubadilika kiwakati. Kati ya masuala ambayo hubadilika ni maudhui, dhamira na matumizi ya lugha. Hii ndiyo sababu kulikuwa na haja ya kufasiri ishara na tamathali katika ushairi na semi za Kivumba. Ushairi na semi za Kivumba ziliteuliwa kimaksudi kwa sababu, fasihi huchipuka kutoka katika jamii mahsusi na huwa na dhima ya kuelezea masuala mbalimbali yanayoihusu jamii husika (Wamitila, 2003). Kama wanavyoshadidia Wamitila (2003) na Atkin (2013), fasihi huashiria ukweli kwa njia ya kutumia lugha kiubunifu ili kumulika masuala muhimu ya kijamii kama vile mazingira na athari zake kwa uchumi na maisha ya kijamii kwa ujumla. Fasihi simulizi hufungamana na maisha ya kila siku ya wanajamii na huonyesha tajriba yao ya kila siku. Ushairi na semi za Kivumba zinadhihirisha athari za kiuchumi na kijamii zinazotokana na kuzorotoka kwa mazingira katika jamii za pwani.

2. Mapitio ya Maandishi

McKay (1975) pamoja na Chiraghdin & Mnyampala (1977) walihakiki baadhi ya methali za Kivumba. Chiraghdin na Mnyampala walinukuu methali tatu zifuatazo:

- Muogova kwambak'aana afanyalo: Aogopaye husemwa hana afanyalo.
- Chungua mwerevu kagwiwa ni tanzi mbovu: Sungura mjanja hunaswa na mtego mbovu
- Kichwa kya kuku kakichukuu mzigo: Kichwa cha kuku hakichukui mzigo (Chiraghdin & Mnyampala, 1977)

Methali huwa na maana husishi na nasibishi. Huwa zinahusu maisha ya wanajamii na kwa hivyo, zinahitaji kufafanuliwa. McKay (1975) alihakiki uamilifu wa methali za Kivumba katika mazingira asilia ya jamii hiyo na kubaini ya kwamba, jamii za pwani zilitumia vipera vya fasihi simulizi kuzungumzia sisa, uchumi, jamii na hata hulka za viongozi kama inavyobainishwa na methali: 'Kwa Wavumba, mkwasi hathaminiwi' (McKay, 1975:325). Kulingana na Ndalul & Kingei (1989), methali ni kati ya vitanzu vya fasihi simulizi ambavyo hufungamana na utamaduni na amali za jamii ya watu. Wanajamii huzitumia kueleza tajriba zao mbalimbali kuhusu maisha. Methali basi huchukuliwa na wanajamii

*Mwandishi Mkuu. Simu: +254723595909; Barua Pepe: sanjaleo254@gmail.com

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.

Nukuu: Leonard S., Evans M. (2025). Uchunguzi Kisemiotiki wa Athari za Kimazingira kwa Uchumi na Maisha ya Kijamii katika Pwani ya Kenya. Jarida la Kiswahili Sanifu, 2(1), 14 – 20.

husika kuwa ni ukweli na ni urithi wa kijamii. Kulingana na methali hiyo, ni juu ya kila mwanajamii wa pwani ya Kenya bila kujali tabaka ama mamlaka yake, kuweka mazingira bora na kuhakikisha jamii yake haiathiriki kwa njia moja ama nyingine. Hilo lilihusu mazingira na tabianchi pia kwani thamani ya mtu ilihusishwa na vitendo kuliko nafasi yake binafsi. Hali hiyo inasisitizwa na methali nyingine: 'Mvaa moja havai mbili na mvaa mbili havai tatu.' (McKay, 1975:325).

Methali hizo zinataja masuala muhimu kuhusu maisha ya kiuchumi na ya kijamii ya Wavumba na watu wa pwani ya Kenya kwa ujumla. Yote ililenga kuwaadilisha wanajamii husika kuhusu kuthamini hali ya jamii zao kuliko kuweka maslahi yao ya kibinafsi mbele. Kulingana na McKay (1975), misemo kama methali katika lahaja ya Kivumba, ilitekeleza wajibu wa kijamii na pia ilikuwa kama nguzo kuu ya kielimu. McKay anakariri kuwa, aliwasikia wazazi wa Kivumba wakiwahimiza watoto kujivunia utamaduni wao na kuepuka ukengeushi: "Nilisikia wazazi wakiwaeleza wana wao, wewe sio Mwarabu bali Mvumba." (McKay, 1975; Sanja na wenzake, 2022). Nidhahiri kwamba, jamii za pwani zimekuwa na mazoea ya kutumia fasihi simulizi kuzungumzia masuala mbalimbali na pia zimekuwa zikitumia kuhifadhi matukio muhimu pamoja na kudumisha utamaduni wao.

Ushairi wa Kivumba umetajwa kama sanaa kongwe na umekuwa ukitumiwa na washairi mbalimbali katika utunzi wa mashairi kwenye fasihi ya Kiswahili. Msami (1982) anatoa kauli ya kwamba, ushairi wa Kivumba ni sanaa ya jadi katika utangulizi wa diwani ya: *Malenga wa Vumba*. Ananukuu:

Kwa kawaida, Wavumba ni washairi wa kale na asili na lugha yao ya Kivumba hupendeza mno ikitumika katika mashairi ya Kiswahili na huweza kumsaidia sana mshairi kwa kufupiza mizani na kurefusha. (Amana, 1982:1-8)

Ni dhahiri kuwa, vipera vya fasihi simulizi kama semi na ushairi vimekuwa vyombo maarufu vya kuzungumzia masuala ibuka katika jamii za pwani na pia kuyahifadhi kwa vizazi vijavyo. McKay (1975), Chiraghdin & Mnyampala (1977) pamoja na Amana (1982) wanashadidia kwa kauli moja ya kwamba, jamii za pwani zina mapisi yanayofanana. Matatizo ama ufanisi wa jamii moja kama vile Kivumba unaakisi taswira kamili ya jamii zote za pwani ya Kenya.

Wamitila (2003) anaeleza ushairi kama:

...sanaa inayotambulishwa na mdundo maalum wa sentensi au vifungu; mpangilio ambao una mdundo maalum au ruwaza fulani inayounda wizani, lugha ya mkato, mafumbo na mpangilio usio wa kawaida wa vifungu fulani. (Wamitila, 2003:104-133).

Kulingana na Wamitila (2003), ushairi hujumuisha masuala muhimu ya kidhamira na kimajukumu. Wamitila (2003) aidha anaeleza dhana ya kwamba, ushairi huwa na sifa ya kuwa na ukiushi wa matumizi ya lugha. Pia, ushairi hutumia tamathali za lugha kwa wingi. Tamathali

hizo hufanya ishara ambazo humhitaji mfasiri wa ishara kuzichanganua ili kuufunua ujumbe unaowasilisha kwa uwazi. Hii ni kwa sababu, fasihi ni sanaa ya lugha (Mbuthia & Iribemwangi, 2014). Lugha ya kiishara huwa na uwezo wa kuwasilisha maana mbalimbali nasibishi katika matini zinazochunguzwa (Bradford, 1997). Isitoshe, lugha ya kiishara hutumiwa kuukoleza ujumbe unaowasilishwa (Senkoro, 1988). Miongoni mwa majukumu ya ushairi ni kufunza na kuelekeza jamii (Arege na Matei, 2005). Hilo linahusisha haja ya kuutumia kudadisi athari za kimazingira kwa uchumi na hali ya kijamii kwa wakazi wa pwani ya Kenya.

Umuhimu wa kufasiri ishara na tamathali ili kuibua maana nasibishi katika ushairi kwa kuzingatia lahaja na mazingira asilia ya utunzi ulibainishwa na Abdulaziz (1979) alipochunguza ushairi wa Muyaka. Tahakiki yake ilidhihirisha kuwa, kila ishara na tamathali za lugha huwa na uamilifu wa kijamii na inaweza kufasirika kikamilifu kulingana na mazingira asilia ya jamii husika. Dhima ya ushairi wa Kiswahili ni kuzungumzia masuala yanayoikumba jamii kwa kutumia lugha yenye mvuto (Mlamali 1980). Kulingana naye, ujumbe na mbinu za uwasilishaji hufungamana na dhamira inayowasilishwa. Kulingana naye, mbinu hufumbata maana nasibishi zinayowasilishwa kisanii. Uhakiki wake unaibua swali: Je, ishara na lugha za kitamathali zina dhima gani katika ufasiri wa ujumbe unaowasilishwa? Swali hilo lilijibiwa na Mbuthia (1991). Mbuthia alichunguza maudhui katika Malenga wa Vumba. Alitumia nadharia ya Uyakiniifu wa Kijamii kubainisha kuwa, maana ya ndani ya mashairi hujitokeza kupitia mbinu mbalimbali za lugha ambazo mtunzi huzitumia. Mbuthia alidhihirisha ya kwamba, kipengele cha muktadha ni muhimu katika ufasiri wa maana nasibishi ya utungo wowote ule wa kishairi. Fasihi huwa na majukumu mengi kwa jamii. Majukumu hayo hayawezi kueleweka bila ufasiri kamili wa ishara na tamathali ambazo ndizo zinafumbata ujumbe wenyewe.

Sanja na wengine (2022) walishughulikia misemo katika lahaja ya Kivumba na kudhihirisha kuwa, ilitumika kuzungumzia masuala kama kuzoroto kwa mazingira, maradhi, kuharibu mazingira, kuharibiika kwa uchumi na ujasiraji mali mbaya. Busara katika jamii hiyo iliandamana na uwajibikaji kwa jamii. Wavumba sawia na wanajamii wengine wa pwani ya Kenya walipenda kuchambua mambo kabla ya kufanya uamuzi wowote kama msembo unavyodhihirisha:

Ukaja na kuni lazima uzikate usiphozikata ukaumwa kuphoi: Ukichana kuni sharti usikate vipande vipande la sivyo ukiugua huponi (Sanja na wengine, 2022:06).

Wavumba walitumia kuni kwa mapishi mara nyingine na hili pia limechangia kudorora kwa misitu katika sehemu nyingi zinazoambatana na bahari. Hiyo ndio maana nasibishi kiseme ya ishara 'kuchana kuni' na 'ukiugua huponi'. Kwa muda mrefu, jamii za pwani zimekuwa zikitumia itikadi za kijamii kuhimiza kuwepo kwa nidhamu katika jamii. Mojawapo ya masuala yanayohitaji nidhamu ni ujasiriamali usioathiri mazingira

na jamii kwa ujumla kama inavyodhihirishwa na: Kizushi cha Mwinyi usi (Sanja na wengine, 2022:08)

Sanja na wengine pia waligundua kuwa, utunzaji wa raslimali haba katika jamii za pwani ya Kenya za kiuchumi ni jambo ambalo lilisitizwa pakubwa:

Kisima kakiuka na ukakiuka kyaja kuuka wewe:
Kisima hakikauki na kikija kukauka kinakuja
kukuauka wewe
(Sanja na wengine, 2022:08)

Maji safi ya ya kisima ya kunywa hayapatikani kwa urahisi katika maeneo mengi katika jamii za pwani ya Kenya. Mji wa Vanga una kisima kimoja pekee kwa wakazi wote. 'Kukauka nawe' ni ishara ya kiseme inayowataka wakazi wa pwani kulinda mazingira na raslimali zao. Mojawapo wa hatua ambazo serikali za kaunti nay a kitaifa imefanya kulinda mazingira ni kupiga marufuku ukataji wa mikoko kama njia moja ya kulinda raslimali (Sanja na wengine, 2022:06).

Kutokana na mapitio ya maandishi, imebainika kuwa, kuna uharibifu mwingi wa mazingira kutokana na shughuli za wanadamu. Mazingira ya Wavumba yanafungamana na mandhari ya bahari. Jamii nyingi za pwani ya Kenya zinaishi katika hali ya umaskini, hawana maji safi ya kunywa, bahari imechafuka na uvuvi umeathirika kutokana na mabadiliko ya kimazingira na tabianchi yaliyopo. Kuna haja ya kupata suluhisho la haraka.

2.1. Nadharia

Makala hii ilitumia nadharia ya semiotiki. Semiotiki ni utohozi wa neno la Kigriki, semeiotikos lenye maana ya ufasiri wa ishara. Neno seme lina maana ya ishara. Ishara ni kitu chochote ambacho kinawasilisha maana na ambayo siyo maana husishi ya ishara yenyewe. Maana isiyokuwa maana husishi yenyewe ya ishara husika ndiyo maana nasibishi ya ishara hiyo. Nadharia ya semiotiki imetumika katika nyanja mbalimbali kama vile: falsafa, isimu, sanaa na fasihi, saikolojia, sanaa ya ujenzi, takwimu, anthropolojia na sosholojia kati ya nyingine. Nadharia ya semiotiki ilianza kushika kasi katika karne ya ishirini kama anavyoshadidia Barry (2002). Inahusishwa na De Saussure (1953) kupitia kazi yake maarufu: A Course in General Linguistic. De Saussure alitoa rai ya kwamba, semiotiki ni ufasiri wa mifumo ya ishara katika maisha. Alichomaanisha ni kwamba, hapana ishara yoyote ambayo haiwezi kuashiria maana nasibishi nje ya muktadha wake wa kawaida.

Barthes (1974) ndiye alikuwa wa karibuni katika miaka ya hamsini, sitini na baadaye kuiendeleza nadharia ya semiotiki baada ya De Saussure (1953), Peirce (1934) na Jakobson (1960). Kulingana na Barthes, ili kupata maana husishi na maana nasibishi ya ishara, ni sharti mfasiri wa ishara azingatia uhusiano uliopo baina ya ishara na kiashiriwa. Barthes (1957) anashadidia suala la kuzingatia mazingira na utamaduni wa kijamii ambamo matini zinazochanganuliwa zimeibukia. Barthes (1957) alitumia kitanzu cha visasili kuelezea dhana yake. Kila kisasili hujikita katika jamii maalumu. Ishara moja inaweza kuwa na maana nasibishi tofauti iwapo ishara

hiyo itafasiriwa katika utamaduni tofauti. Hata katika utamaduni mmoja, kuna uwezekano ishara hiyo hiyo ikawa na maana tofauti. Kulingana naye, mielekeo maarufu ya kitamaduni mara nyingi ndiyo hutumiwa kufasiri ishara kwa njia inayokubalika na wengi. Barthes alitumia mfano wa ishara ya mvinyo wa Kifaransa kudhihirisha kauli yake. Mvinyo ni ishara ya kitamaduni inayoashiria ufahari, ustawi na ustaarabu katika jamii ya Kifaransa. Kulingana naye, tabaka lenye ushawishi huweka mielekeo ya kufuatwa na jamii. Hii ina maana kuwa, ishara inaweza kuwa ileile lakini maana nasibishi zikawa tofauti kutegemea mfasiri wa ishara, dhamira na maarifa ya kijamii alionayo mfasiri wa ishara. Mfasiri wa ishara basi anahitaji kutumia hekima pamoja na maarifa ya kijamii kuifasiri ishara inayochanganuliwa kwa kuzingatia elimu ya jamii hiyo. Kauli hiyo ya Barthes (1957) ilikuwa msingi wa msimbo wa kirejelezi.

Barthes (1957) alitazama matini zote kama mfumo wa ishara ambazo zinahitaji ufasiri ili kuibua maana nasibishi (Barry, 2002). Barthes (1964) alihimiza msomaji wa matini kung'amua maana ya ndani ya matini kwa kutumia vielekezi mbalimbali vilivyomo katika matini zenyewe. Kulingana naye, kila msimbo ni sauti ambayo imefungamanishwa na matini zinazochunguzwa. Kwa hivyo, kila ishara katika ushairi ama semi inatakiwa kufasiriwa kikamilifu ili maana yake nasibishi iwe dhahiri kwa msomaji wa matini husika. Barthes (1974) alijadili ya kwamba, hata pale ambapo msomaji wa matini za kifasihi anasoma kwa njia ya kujiburudisha, kuna kiwango ambapo hufika akabaini maana nasibishi ya matini husika katika fikra zake. Barthes aliita hali hiyo, ung'amuzi huru. Yaani kuna wakati ambapo mfasiri wa ishara hupata maana ambayo iko kando sana na mazoea yaliyopo. Katika usomaji wa aina hiyo, msomaji wa matini anatafuta vielekezi ambavyo vitamwongoza katika kufikia maana nasibishi ambayo iko nje ya muktadha uliozoeleka. Barthes (1957), Barthes alijadili kuwa, mielekeo ya kijamii huelekeza namna lugha na mtindo wa uandishi hutumiwa na mwandishi husika kufikia malengo yake. Baadhi ya ishara zinaweza kufasirika tu kwa kupimwa kwenye mizani ya mielekeo iliyopo. Maana za ishara hubadilika kulingana na mabadiliko ya kiwakati pamoja na matarajio ya wanajamii (Barthes, 1974). Pia, baadhi ya ishara hazihitaji ufafanuzi zaidi ya maana husishi ya ishara. Barthes alipendekeza msomaji wa matini za kifasihi kutenganisha matini na mwandishi wake katika Barthes (1967).

Mjadala ulitumia mihimili iliyotokana na misimbo ya kiishara, kisemi na msimbo wa kirejelezi kulingana na Barthes. Msimbo wa kirejelezi hujengwa kwa misingi ya viashirii vya kitamaduni (Wamitila, 2002b). Msimbo wa kirejelezi basi huhusu namna msomaji wa matini za kifasihi huishia kufasiri ishara na kupata maana nasibishi kutokana na tajriba yake ya muda mrefu kutoka katika maarifa ya kijamii (kitamaduni), mielekeo yake ama itikadi zake (Barthes, 1974). Ishara za kitamaduni huwa zinaeleweka na mfasiri wa ishara tayari na hujenga uhalisia maalumu katika fikra zake. Mwenyeji wa Kivumba akipatana na msembo kama: 'Ni aibu mwanaharusi kutembea uchi siku ya harusi,' anaweza

kuhusisha na jamii husika na kupata maana nasibishi inayolengwa. Yaani, mfasiri wa ishara anaweza kutambua moja kwa moja iwapo ishara ni ya kidini, kitamaduni ama ya kisayansi. Msimbo wa kiishara hutumiwa kurejelea mfumo wa ishara ambazo huashiria maana husishi na nasibishi ya ishara. Ishara inaweza kuwa ni kitu dhahiri, mazingira ama usemi fulani unaoashiria maana nasibishi. Huhusu namna mfasiri wa ishara katika matini za kifasihi huunda wazo (maana) katika fikra zake na jinsi huishia kung'amua maana nasibishi ya ishara. Ili kutambua aina hii ya ishara, mfasiri wa ishara anastahili kutathmini muktadha na dhima ya ishara husika wakati wa kufasiri maana nasibishi ya ishara.

Msimbo wa kiishara basi huhusu namna mfasiri wa ishara huunda maana husishi ya ishara katika fikra zake na jinsi maana hiyo humwongoza kwenye maana nasibishi ya ishara. Yaani, katika aina hii ya ishara, kuna uhusiano baina ya maana husishi ya ishara na maana nasibishi. Msimbo wa kiseme hutumiwa kuelezea mfumo wa ishara zenye kuleta maana nasibishi katika matini zinazochunguzwa. Msimbo huu pia huitwa msimbo wa kisemantiki. Ishara za kiseme huelezea matukio, wahusika ama mandhari ili kuibua maana nasibishi mbalimbali kwa njia ya uashiraji. Matini zenyewe humwelekeza msomaji kwenye maana nasibishi. Maana nasibishi huwa zimetapakaa ndani ya matini yote na hufanya viashirii fulani katika fikra za mfasiri wa ishara na kumfanya kung'amua taswira fulani ya kiashiriwa. Maana nasibishi inaweza kutokana na majukumu ya ishara husika ama viashiria vyake vingine katika matini. Hii ndiyo tahakiki ambayo makala hii ilizingatia katika uchanganuzi.

3. Mjadala na Matokeo

Uchambuzi Ishara za kiseme huibua maana nasibishi mbalimbali za ishara kwa njia ya uashiraji. Msimbo wa kiishara kwa upande wake, huchanganua mfumo wa ishara ambazo huashiria maana husishi na nasibishi ya ishara kila mara zinapochunguzwa. Ishara inaweza kuwa ni kitu dhahiri, mazingira ama usemi fulani unaoashiria maana nasibishi. Katika kujadili athari za kimazingira na kiuchumi, ushairi na semi za Kivumba ulihitajika ili kutoa data ambayo ilichanganuliwa katika makala hii.

3.1. Athari za Kimazingira kwa Ajira

Mabadiliko hasi ya kimazingira imeathiri jamii za pwani ya Kenya kiuchumi pakubwa. Wakazi wengi hawana ajira na mifumo ya kijamii imeanza kuvurugika. Katika shairi lenye mada: Wasini ([Sanja na wengine, 2022](#)) tunasoma:

Kazi zenu za Wasini, ni za mashaka
Paka rwende baharini, ndio mke achaphika
Au yaje Majapan Kisite kuyaphilika
Mji weru wa Wasini ni mji wenye Baraka.

Siyo rahisi kupata kazi huku Wasini, nisharti mtu aende baharini kuvua ndiposa mke apate riziki nyumbani. La, sivyo hadi waje wageni (watalii kama Majapani) kwenye mbuga ya Kisite ndipo tupate riziki. Mji wetu wa Wasini ni Mji wa Baraka. (Tafsiri yetu).

Uzalendo unafanya wakazi wa Wasini na Shimoni na pwani kwa ujumla kutoyachukia mazingira yao kwani hawana mahali pengine pa kwenda. Hiyo ndiyo maana nasibishi ya kisemiotiki ya: Mji wetu wa Wasini ni Mji wa Baraka. Mshairi inaonyesha hali ya kutamaukiwa katika jamii za pwani ya Kenya. Mojawapo wa athari za kimazingira ni kuibuka kwa njaa, umaskini na kukosa riziki nyumbani. [Barthes \(1957\)](#) anasema kwamba, ishara moja inaweza kuwa na maana nasibishi tofauti, iwapo ishara hiyo itafasiriwa katika utamaduni tofauti. Anaongezea kuwa, hata katika utamaduni mmoja, kuna uwezekano wa ishara hiyohiyo kuibua maana nasibishi tofauti kabisa na jinsi ilivyozoeleka. Kulingana naye, mielekeo maarufu ya kitamaduni mara nyingi ndiyo hutumiwa kufasiri ishara kwa njia inayokubalika na wengi. Jamii nyingi katika pwani ya Kenya haziwezi kumudu mlo na lishe bora kwa familia kulingana na mshairi wa Kivumba. Samaki hawapatikani kama. Familia nyingi zimekuwa maskini na zinaishi kwa kutegemea kupata riziki kwa njia za kubahatisha kwa mfano iwapo watalii watafika katika sehemu za mbuga kama Kisite ama la. Mshairi anasisitiza anaposema: Au yaje Majapan Kisite kuyaphilika. Ni dhahiri kwamba, jamii nyingi za pwani ya Kenya zinaishi bila tumaini na zipo katika shinikizo la kiuchumi na kimazingira mara kwa mara.

3.2. Athari za Kimazingira kwa Asasi ya Ndoa

Athari kuu ya kimazingira pwani ya Kenya ni kuvurugika kwa asasi ya ndoa kutokana na umaskini na kukosa maslahi ya kila siku nyumbani. Kulingana na shairi, hali hiyo haikuwepo hapo awali bali imesababishwa na mabadiliko yanayoshuhudiwa sasa:

Wanawake wa zamani, sasa wanageuka
Kwa kaa majumbani, hata kwenye mabinka
Sasa wende madukani, bila hata kujifinika
Mji weru wa Wasini ni mji wenye Baraka

Kutokana na ugumu wa kiuchumi na kijamii, ndoa imeathirika. Utamaduni wa mke kuketi nyumbani, kujistiri na kutotangamana na umma umevunjwa na kuibua taharuki katika jamii za pwani. Msimbo wa kiishara hutumiwa kurejelea mfumo wa ishara ambazo huashiria maana husishi na nasibishi ya ishara. Ishara inaweza kuwa ni kitu dhahiri, mazingira ama usemi fulani unaoashiria maana nasibishi. Kisemiotiki, kuna vita vya kiuchumi majumbani baina ya wanaume na wanawake kwa sababu shughuli ambazo wanaume walikuwa wakifanya ili kuleta riziki nyumbani, sasa zinafanywa na kina mama. Kutokana na hali hiyo, wanawake wamepata uhuru zaidi na kukaidi mila na desturi. Kwa muda mrefu, shughuli kuu ya kiuchumi katika jamii za pwani ilikuwa ni uvuvi. Hata hivyo, imeathirika na huenda ndicho chanzo kikuu cha ugomvi katika ndoa na kuvunjika kwa miko kama msemu unavyodhihirisha:

'Tumbi ya mbilikiza kaijaa swii': Kapu la mvuvi halijai samaki

Methali huwa na dhima nyingi katika jamii ikiwemo kudumisha mapisi na utamaduni ([Wamitila, 2003](#)). Ishara za, 'Tumbi'(kapu) na 'kaijaa' (haijai) ni za kiseme

ambazo zinaibua maana nasibishi ya kwamba, iwapo mazingira ya bahari haitahifadhiwa na kutunzwa tena, jamii za pwani zitazidi kuathirika kiuchumi na kijamii hata zaidi.

3.3. Athari za Kimazingira kwa Maji ya Kunywa na Afya ya Wakaz

Maeneo mengi ya pwani ya Kenya yana uhaba wa rasimali muhimu na hasa maji ya kunywa. Maeneno mengi hayana visima vya maji safi ya kunywa na vilivyoko huchafuliwa na maji ya bahari kunapokuwa na mafuriko. Eneo kama la Vanga, lina kisima kimoja tu kwa wakazi wote wa huko (Sanja na wengine, 2022). Katika shairi lenye mada ya: Wasini, mshairi anakariri:

Maji yetu ya mabirika, mara nyingi hukauka
Yakiisha twenda Shimoni, kuyapata ni mashaka
Au yanaletwa na meli, yana kutu na taka
Mji wetu wa Wasini ni mji wenye Baraka

Eneo la Wasini limezungukwa na bahari na sio rahisi kupata maji safi ya kunywa pamoja na bidhaa nyinginezo. 'Maji yetu ya mabirika, mara nyingi hukauka, yakiisha twenda Shimoni, kuyapata ni mashaka. Mshororo huu ukisasiriwa na msimbo wa kiishara unaibua maana nasibishi kuwa, sehemu nyingi za pwani zinakabiliwa na ukame wa mara kwa mara kutokana na mazingira duni. 'Kukauka' na 'kuendea Shimoni' kisemiotiki kunaibua maana nasibishi ya kwamba, maji safi ya kunywa huletwa kutoka sehemu za bara na kuhifadhiwa wakati mwingine kwenye visima. Vinapokauka, hubidi wananchi wengi wa pwani kugharamika ndiposa wayapate kutoka sehemu za mbali kama Shimoni. Kulingana na Sanja na wengine (2022), Wavumba bado huenda katika sehemu za mbali kama za Vumba Kuu kwa shughuli za ukulima ndiposa wapate riziki na chakula.

Maana nasibishi ndiyo Barthes anaiita kisemiotiki, muundo wa ndani wa ishara (Barthes, 1974). Muundo wa ndani humdhibiti mfasiri wa ishara na huathiri namna anavyofasiri ishara husika: 'Maji ya mabirika' 'kuletwa na meli' na 'yakiisha twenda Shimoni' ni ishara za kiiashiria. Wapwani wengi wanaoishi kwenye visiwa kama Wasini, hutumia gharama nyingi ili kusafirisha maji safi ya kunywa kutoka sehemu za bara. Hali hiyo imewafanya wengi kuwa maskini na kuvumilia mazingira duni na hali mbaya ya maisha. Vilevile, kuna suala la afya ambalo linaambatana na mazingira mabovu ya wapwani. Maji yanayolewa na meli ama mashua huwa machafu na hivyo kuhatarisha afya za wakazi. Hiyo ndiyo maana ya kisemiotiki ya: 'Au yanaletwa na meli, yana kutu na taka.'

Eneo la Vanga lina kisima kimoja pekee (Sanja na wenzake, 2022). Kulingana na Barthes (1964), tabaka lenye ushawishi huweka mieleleko ya kufuatwa na jamii kwani huwa lina ushawishi kwa wengi. Hii ina maana kuwa, ishara inaweza kuwa ileile lakini maana nasibishi ikawa tofauti kutegemea mfasiri wa ishara, dhamira ya ishara ama maarifa ya kijamii alionayo mfasiri wa ishara husika kama inavyodhihirishwa na msembo wa Kivumba: 'Kisima kakiuka na ukakiuka kyaja kuuka wewe': 'Kisima

hakikauki na kikija kukauka kinakuja kukukausha wewe pia.'

Mfasiri wa ishara basi anahitaji kutumia hekima pamoja na maarifa ya kijamii ya muda mrefu kuifasiri ishara husika kwa kuzingatia elimu ya jamii hiyo. Kauli hiyo ya Barthes ilikuwa msingi wa msimbo wa kirejelezi. Maeneo mengi ya pwani hayana rasimali nyingi. Hiyo ndiyo maana ya kirejelezi ya: 'Kukauka nawe'. Wapwani wenyewe wanastahili kutunza chemchemi za maji na mazingira kwa ujumla. Kiseme, ni ishara ambayo inasisitiza kwamba, wakati umefika ambapo jamii za pwani zinastahili kutumia uchumi wa kijani.

3.4. Athari za Kilimo cha Mashamba Makubwa kwa Mazingira

Chanzo cha kuzorota kwa mazingira pwani ya Kenya ni masuala ya kiistoria. Waarabu walianzisha tawala na biashara ya mashamba makubwa 1868. Waarabu walianzisha kilimo cha mashamba makubwa na biashara nyinginezo bila kuzingatia utunzaji wa mazingira. Hadi kufikia mwaka wa 2012 wakati ambapo serikali ya Kenya ilipiga marufuku ukataji wa mikoko, hali ya mazingira ilikuwa imeharibika pakubwa (Sanja na wengine, 2022). Wapwani wengi hawakuhusishwa kikamilifu katika shughuli za kibiashara na hatimaye utunzaji wa mazingira na ndiposa wengi wao walichukizwa na hulka za walioathiri mazingira kama lakabu ya Kivumba inayoashiria.

3.5. Kizushi cha Mwinyi

Kulingana na msimbo wa kiseme, 'mwinyi' ni ishara inayoibua maana nasibishi kurejelea watu waliohodhii mali na mamlaka na kuyatumia vibaya dhidi ya watu wa pwani ya Kenya bila kujali hali ya kimazingira kama walivyofanya Waarabu. 'Kizushi' kisemiotiki ina maana nasibishi ya kuwa kibaraka cha watawala. Maana ya kina ni kuwa, baadhi ya watu wenye uwezo katika jamii za pwani wamekuwa wakishirikiana na watu wenye uwezo kutoka nje ya pwani kuathiri mfumo mzima wa maisha na mazingira katika pwani ya Kenya. Waarabu waliharibu mazingira kwa kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa na kudumisha mfumo wa kibepari; mfumo ambao unaruhusu wachache kumiliki nyenzo za uzalishaji wa mali.

Siyo Waarabu pekee walioathiri jamii za pwani bali pia kulikuwa na wakoloni. Baadhi ya misemo ya Kivumba iliibuka kutokana na mtagusano wa jamii za pwani ya Kenya na wakoloni. Mtagusano kati ya wapwani na wakoloni hao uliwadhalilisha wapwani wengi kiuchumi na kimazingira na kusababisha ukengeushi kama msembo ufuatao unavyoashiria:

Wenyewe rwaweza kupanga meza kama Waingereza:
Wenyewe tunaweza kuandaa meza kama Wazungu
(kujifanyia na kujiamulia hatima yetu)
(Tafsiri yetu)

Kwa mujibu wa msimbo wa kiseme, mfasiri wa ishara huongozwa na ishara yenyewe kwenye maana nasibishi (Barthes, 1957). 'Wenyewe rwaweza kupanga meza' ikifasiriwa kisemiotiki inaibua maana nasibishi kuwa, baada ya Kenya kupata uhuru wa bendera, jamii nyingi

za pwani ziliendelea kukandamizwa kisiasa. Hadi kufikia mwaka wa 2013, maeneo ya kusini mwa Mombasa kama Vanga hayakuwa na barabara ya lami na mikoko ilikuwa bado inakatwa na kuuzwa ng'ambo licha ya serikali kusitisha biasha hiyo (Sanja na wengine, 2022). Eneo la Vanga na Shimoni yanashuhudia mafuriko ya mara kwa mara ya bahari kutupa nje maji yake kutokana na kuchafuliwa kwa bahari na kukatwa kwa mikoko.

3.6. Athari za Ekolojia kwa Mazingira ya Pwani

Ekolojia ni uhusiano baina ya viumbe hai na viumbe vingine. Katika maeneo mengi ya pwani, uhusiano huo umeathirika kutokana na mazingira kuharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu. Wadudu ni sehemu muhimu ya mazingira ya mwanadamu mbali na mimea. Nyuki ambao awali walitumia miti na maua ambayo yalikuwa mengi kuunda asali, sasa wameathirika. Katika shairi, Wajenzi, mshairi wa Kivumba anasema:

Nyuki uvivu hawana wanatahadhari
Njaa kazi zao dana dana haraka na kutambaa
Masega yajijazana mara asali ya jaa umkarimu
mrina aje kuitwaa.

'Nyuki' ni ishara ya kirejelezi kulingana na msimbo wa kirejerezi (Barthes, 1997). Ni dhahiri kuwa, mandhari ya pwani yameathirika na umaarufu wake kupotea na hayavutii tena. Isitoshe, faida iliyotokana na kuishi vyema na viumbehai vingine kama nyuki na kurina asali, ni tukio ambalo halifanyiki tena. Hali hiyo imepunguza viteka uchumi kwa watu wa pwani. Jamii nyingi zinakabiliwa na njaa na ukosefu kutokana na kwamba, athari za kiekolojia ni dhahiri katika maeneo mengi ya pwani ya Kenya.

3.7. Athari ya Mazingira na Mafuriko ya Mara kwa Mara

Mazingira ya jamii nyingi za pwani yanafungamana na mandhari ya bahari. Wakazi wa maeneo ya kusini mwa Mombasa kama Vanga, Shimoni na Wasini wamepakana na Bahari ya Hindi na mara kwa mara wanakumbana na mafuriko bahari inapojaa ama kupigwa na mawimbi. Hali hiyo inaelezwa kupitia misemo kama:

- Maji ya kinondo: Kutapakaa kwa maji: Mvua nyingi (kuzidiwa na mambo)
- Bahari kupwa: Bari kufurika na kuyamwaga maji nje ya mipaka yake
- Msimu wa kusi: Msimu wa mvua nyingi

Kulingana na Barthes (1981), baadhi ya ishara zinaweza kufasirika tu kwa kupimwa kwenye mizani ya mielekeo iliyopo. Anaongezea kuwa, maana za ishara hubadilika kulingana na mabadiliko ya kiwakati pamoja na matarajio ya wanajamii. Pia, baadhi ya ishara hazihitaji ufafanuzi zaidi ya maana husishi ya ishara. 'Bahari kupwa: Bari kufurika na kuyamwaga maji nje ya mipaka yake' ni hali ya kawaida kwa wakazi wa pwani wanaopakana na bahari. Hata hivyo, hali hiyo imekuwa ikiongezeka kupita kiasi kadiri ambavyo mazingira yanazidi kuharibiwa kutokana na shughuli za watu kama kutupa uchafu baharini pamoja na kukata miti. Katika sehemu ya Vanga, mara nyingi maji ya bahari hujaa na kutoka nje. Yanaporejea, mengine husalia nje kwa muda

mrefu na kuathiri maisha ya wakazi kwa kuvutia nyoka, wadudu kama mbu na hata kuvuruga makazi ya wengine. Eneo la Vanga mara nyingi hukumbwa na mafuriko kutokana na mvua ama kuchafuka kwa bahari. Hali hiyo hutataiza usafiri wa kutoka maeneo mengine kwa watu ambao wanataka kufika huko kutoka miji kama Mombasa na Lungalunga (Sanja na wengine, 2022).

4. Hitimisho

Mjadala katika makala hii ulihitimisha kwamba, athari za kimazingira katika jamii za pwani ya Kenya ni nyingi kulingana na ushairi na semi za Kivumba. Wakazi wengi hawana ajira, kumudu riziki za nyumbani ni ngumu na wanaishi katika viwango vibaya vya umaskini. Kutokana na kuchafuliwa kwa bahari, uvuvi umeathirika na samaki hawapatikani kama kitambo. Familia nyingi zinapatashida kujikimu kwa chakula nyumbani. Ushairi na semi pia umedhihirisha kuwa, mifumo ya kijamii ya kijadi inayohusishwa kidini na kitamaduni na asasi ya ndoa imeanza kuvurugika mno. Wanawake wameanza kutoka nje ya ndoa kwenda kujitafutia riziki kinyume na ilipokuwa pale awali. Kwa sababu hiyo, kuna mikwaruzano ya kindoa katika jamii za pwani ya Kenya. Aidha, kupitia mjadala, imebainika kuwa, maeneo mengi ya pwani hayana maji safi ya kunywa na yanayoletwa kutoka katika sehemu za bara huwa chafu, humalizika haraka na hivyo kuwasababishia wenyeji gharama na hatari ya kupata maradhi. Maeneo mengi kama Vanga, Shimoni na Wasini yana uhaba wa visima vya maji safi. Ilibainika vilevile ya kwamba, kutokana na kuharibika kwa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kuna mafuriko katika maeneo mengi ya pwani.

Marejeleo

- Abdulaziz, B. H. (1979). *Muyaka: Nineteenth Century Swahili Popular Scholar Poetry*. Nairobi. Kenye Literature Bureau.
- Atkin, A. (2013). *Peirce's Theory on Signs*. Stanford Encyclopedia of Philosophy.
- Amana, B. (1982). *Malenga wa Vumba*. Nairobi. Oxford University Press.
- Arege, T & Matei, A. (2005). *Kunga za Kiswahili 3: Kitabu cha Mwanafunzi*. Nairobi. Focus Publishers.
- Barthes, R. (1953). *Writing Degree Zero*. Hill & Wang.
- Barthes, R. (1957). *Mythologies*. New York. Hill & Wang.
- Barthes, R. (1967). *The Death of the Author*. Hill & Wang.
- Barthes, R. (1964). *Elements of Semiology*. New York. Hill and Wang.
- Barthes, R. (1974). *S/Z*. (R. Miller, Trans.) United Kingdom. Blackwell Publishing Ltd.
- Barthes, R. (1997). *Image-Music-Text*. S. Heath (Ed). *The Journal of Aesthetics and Criticism*. (Vol. 37), (uk. 220.) Hill and Wang.
- Barthes, R (1981). "Theory of the Text" Ian Macleod (Trans), Katika R. Young (ed.) *Untying the Text*. London. Routledge.
- Barry, P. (2002). *Beginning Theory: An Introduction to*

- Literary and Cultural Theory. Manchester.
Manchester University Press.
- Bradford, R (1997). *Stylistics. The Critical Idiom*. London.
Routledge.
- Chiraghdin, S & Mnyampala, M. (1977). *Hisitoria ya Kiswahili*. Nairobi. Oxford University Press.
- De Saussure, F.(1959). *Course in General Linguistics*.(Trans. Wade,B) Philosophical Library.
- Jakobson, R. (1960). "Closing Statement: Linguistics and Poetics," in *Style in Language* (ed). Thomas Sebeok.
- Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London. Longman Group Limited.
- Mbuthia E. M. & P. I. Iribemwangi. (2014). Analysis of Stylistic Trends in Published Kiswahili Short Story Genre. *Journal of Education and Practice*: www.iiste.org ISSN 2222-1735 (Paper). Vol.5, No.8, 2014. (uk. 32).
- Mckay, W. F (1975). "Pre-colonial history of the Southern Kenyan Coast". Unpublished PhD, dissertation. Boston University.
- Mlamali, M (1980). *Inkishafi*. Nairobi. Longman Kenya Ltd.
- Msami,H.(1982). *Utangulizi. Katika Malenga wa Vumba*. Oxford University press.
- Ndalu,E. &King'ei,K.G. (1989). *Kamusi ya Methali*. Nairobi EAEP.
- Peirce, C. S. (1934). *Collected papers: Volume V. Pragmatism and pragmaticism*. Cambridge, MA, USA: Harvard University Press.
- Sanja, L.W.L & Others. (2022). 'Siasa, Uchumi na Ustawi wa Jamii: Mtazamo wa Kisemiotiki wa Ushairi wa Kivumba.' *Mwanga wa Lugha (J.K.L.K)*. Chuo Kikuu cha Moi. Juzuu7 Na .1 April uk 89-103, 2022.
- Senkoro, F. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia naTahakiki*. Dar es Salaam. Dar es Salaam. University Press.
- Wales, K (2011). *A Dictionary of Stylistics*. 3rd Edition. London. Routledge.
- Wamitila, K .W. (2002 b). *Kamusi ya Misemo na Nahau . Lulu za Lugha*. Longhorn Publishers.
- Wamitila, K .W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publishers